# UJUMBE WA SULUHU

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi

Ujumbe wa Suluhu
Tafsiri ya Kiswahili ya: Paighame Sulha (Kiurdu)

Mwandishi:
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

Mfasiri: Sheikh Yusuf Athumani Kambaulaya

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): 1908
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2017

© Islam International Publications Ltd.

Kwa Maelezo Zaidi:
Tanzania:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

Kenya:
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

ISBN: 978-1-84880-556-9

# Jalada la chapa ya mara ya kwanza

ٹائیٹل بار اول

الصُّلح خیر

# پیغامِ صُلح

جو

ہندوستان کے دو بڑے مذہب یعنے ہندو ازم اور اسلام میں مصالحت
کرانے کے لئے اعلیٰحضرت حضرت حجۃ اللہ المسیح الموعود والمہدی المعہود علیہ الصلوٰۃ
والسلام نے اپنی زندگی کے آخری دو تین دنوں میں لکھا اور جو معزز ہندو و
مسلمانوں کے ایک عظیم الشان جلسہ میں بمقام پنجاب یونیورسٹی ہال لاہور
بتاریخ ۲۱ ماہ جون ۱۹۰۸ء پڑھا گیا۔

مطبوعہ مطبع نولکشور پریس لاہور

## Jalada la chapa ya kwanza

Suluhu ni Bora

# Ujumbe wa suluhu

Ambao

Hadhrat Hujjatullah Masihi Mau'udi na Mahdi Aliyeahidiwa a.s. aliuandika katika siku mbili, tatu za mwisho wa maisha yake kwa kuzisuluhisha dini mbili kubwa za India, Ubaniani na Uislamu, ambao ulisomwa katika hadhara kubwa ya waheshimiwa Mabaniani na Waislamu ndani ya ukumbi wa Panjab University, Lahore, mnamo tarehe 21 mwezi Juni 1908,

nao ulipigwa chapa

Katika Matbaa Naolkishvar, Lahore

## Neno la Mwenezi

Dawati la Kiswahili lina heshima ya kuwaletea wasomaji tafsiri ya kitabu kingine tena cha Seyidna Ahmad[as], Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya.

Kitabu chenyewe, Paighame Sulha (Ujumbe wa Suluhu), kiliandikwa na Seyidana Ahmad[as] mnamo Mei mwaka 1908 ambamo aliyaelekeza mataifa mawili makubwa ya Bara Hindi, Waislamu na Mabaniani, Kuondolea mbali chuki baina yao na kukaa kwa amani na kuheshimiana.

Sheikh Yusufu Athumani Kambaulaya alikifasiri kitabu hiki kwa Kiswahili kwa uangalifu. Kisha Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, Amiri na Mbashiri Mkuu wa zamani wa Tanzania akaidurusu na kabla ya kuipeleka mtamboni kuchapisha nikaisoma na kuisogeza karibu na matini ya Kiurdu iwezekanavyo.

Sheikh Ansar Hussain na Sheikh Nasr Ahmad Bhatti nao wakapanga herufi za chapa, na Syed Tanwir Mujtaba akafanya kazi ya *fometi*.

Mwenyezi Mungu Awapatie hao wote malipo bora hapa dunia na huko Akhera.

Mola Mtukufu Awajalie wasomaji wanufaike barabara na kitabu hiki. Amin

Jamil R. Rafiq
Wakilut-Tasnif
Tahrike Jadid
Rabwah. Pakistan
19.03.2017

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ [1]

نَحْمَدُهٗ وَنُصَلِّيْ عَلٰى رَسُوْلِهِ الْكَرِيْمِ [2]

Ee Mungu wangu Mweza, Ee Mwongozi wangu mpendwa! Utuonyeshe njia ile ambayo kwayo wakweli wanakufikia, na Utuepushe na njia zile ambazo makusudio yake ni tamaa za nafsi tu au chuki au bughudha au uchu na tamaa ya dunia.

Amma ba'du, enyi wasikilizaji! Sisi sote, Waislamu na Mabaniani, juu ya mamia ya hitilafu tunashirikana katika kumwamini yule Mungu Ambaye ndiye Mwumbaji na Mmiliki wa dunia, na kadhalika sisi sote twashirikiana katika jina binadamu, yaani sisi sote tunaitwa binadamu. Na vilevile kwa sababu ya kuwa wakaaji wa nchi moja, tu majirani wenyewe kwa wenyewe. Hivyo basi, ni faradhi yetu kwamba kwa moyo safi na kwa nia njema tuwe marafiki sisi kwa sisi, na katika matatizo ya kidini na kidunia tuhurumiane, na tuhurumiane kiasi hiki kana kwamba kila mmoja wetu yu viungo vya mwingine.

Enyi wananchi! Dini ile siyo dini ambamo hamna mafundisho ya kuhurumiana kwa jumla. Na mtu yule

---

1 Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu. Mwenezi.

2 Tunamhimidia Yeye na tunamsalia Mtume wake Mtukufu. Mwenezi.

si mtu asiye na huruma ndani ya tabia yake. Mungu wetu Hakuweka tofauti yoyote kwa taifa lolote lile, mathalan, nguvu zile zile za kibinadamu walizopewa watu wa kale wa India, nguvu zote hizo walijaliwa Waarabu, Waajemi, Wasiria, Wachina, Wajapani na mataifa ya Ulaya na ya Amerika pia. Ardhi ya Mungu ni kama sakafu kwa wote, jua lake mwezi na nyota kadha zinafanya kazi ya taa zing'aazo na hutoa huduma zingine pia kwa wote. Elementi Alizoumba, yaani hewa, maji, moto, vumbi na kadhalika vitu vingine vilivyoumbwa naye — nafaka, matunda, dawa na kadhalika — mataifa yote yanafaidika navyo. Hivyo, khulka hizi za Mungu zinatufundisha somo kuwa sisi pia tuwatendee wanadamu wenzetu ukarimu na wema, wala tusiwe na mioyo finyu na roho ndogo.

Marafiki!! Eleweni kwa yakini kuwa kama miongoni mwa mataifa yetu mawili, taifa mojawapo halitastahi khulka za Mungu, na litakuwa na mienendo kinyume cha khulka Zake tukufu, basi taifa hilo litaangamia haraka, na siyo hilo lenyewe tu bali litaiangamiza hata dhuria yake pia. Tangu dunia ilipoumbwa, watu wema wa nchi zote wameendelea kutoa ushahidi kuwa kufuata khulka za Mungu ndiyo maji ya uhai kwa kudumisha binadamu, na maisha ya wanadamu kimwili na kiroho yanategemea jambo hili kuwa

wazifuate khulka zote takatifu za Mungu ambazo ndizo chemchemi za usalama.

Mwenyezi Mungu Ameanzia Kurani Tukufu na Aya hii iliyomo ndani ya Sura Al-Faatiha, اَلۡحَمۡدُ لِلّٰہِ رَبِّ الۡعٰلَمِیۡنَ[3] yaani sifa zote kamili na takatifu zinamhusu Mungu Ambaye ni Mola wa walimwengu wote. Neno ulimwengu linajumuisha mataifa yote, zama zote na nchi zote mbalimbali. Kwa aya hii Kurani Tukufu ilianzishwa. Kwa kweli huku ni kukanusha fikara ya wale wanaoukomesha mpaka kwa mataifa yao tu ulezi na ukarimu wa Mungu ambao ni kwa ajili ya watu wote, na wanayadhania mataifa mengine kana kwamba si viumbe wa Mwenyezi Mungu, kana kwamba baada ya kuwaumba hao Mungu Akawatupa kama takataka, au Amewasahau, au (Mungu Apishe mbali) hao sio viumbe wake. Ni kama vile wanavyofikiria Wayahudi na Wakristo mpaka leo kuwa manabii na mitume wote wa Mungu waliokuja walitokea kutoka koo za Wayahudi tu, na Mungu Akawa Ameyakasirikia mataifa mengine kiasi hiki kwamba hata baada ya kuwaona wamo ndani ya upotofu na mghafala Hakuwajali kabisa, kama ilivyoandikwa ndani ya Injili pia kuwa Hadhrat Masihi[as] alisema kwamba mimi nimekuja kwa ajili ya

[3] Al-Faatiha, 1:2

kondoo tu wa Israeli. Hapa tunaongea kimuhali tu kuwa baada ya dai la uungu mawazo finyu ya namna hii ni jambo la kushangaza sana. Je Masihi alikuwa ni Mungu wa Waisraeli tu na hakuwa Mungu wa mataifa mengine hata kwamba akapata kutamka mdomoni mwake kuwa mimi sihusiki na urekebisho na mwongozo wa mataifa mengine.

Ilmuradi, itikadi ya Wayahudi na Wakristo ni hii hii kuwa Manabii na Mitume wote walikuwa wakija kutoka ndani ya ukoo wao, na vitabu vya Mungu vimeendelea kuteremka ndani ya ukoo wao. Na kisha kwa mujibu wa itikadi za Wakristo, mfululizo wa ufunuo na wahyi uliishia kwa Bwana Yesu, na ufunuo wa Mungu ukapigwa muhuri.

Waaria pia wanafuata mawazo hayo. Yaani, kama vile Wayahudi na Wakristo wanavyouwekea mipaka unabii na ufunuo mpaka kwa nyumba ya Israeli tu na wanayanyima mataifa mengine yote heshima ya kupata ufunuo, ndivyo Waaria wanavyokuwa na itikadi hii hii kwa bahati mbaya, yaani wao pia wana itikadi kuwa silsila ya wahyi na ufunuo wa Mungu haujavuka eneo la India. Daima Rishii (manabii) wanne huteuliwa kutoka katika nchi hii hii, na daima Veda tu inashuka mara kwa mara, na daima lugha ya Kisanskiriti tu imewekwa mahususi kwa ajili ya kuifunulia.

Ilmuradi, mataifa hayo mawili hayamtambui Mungu kuwa ni Mola wa walimwengu, waila haionekani sababu yoyote kuwa Mungu Anayeitwa Mola wa walimwengu siyo tu Mola wa Waisraeli au Mola wa Waariya, kwa nini anafanya uhusiano wa kudumu na taifa moja mahususi, jambo ambalo linaonyesha upendeleo wa wazi wa upande mmoja. Hivyo basi, kwa kukanusha itikadi hizi Mwenyezi Mungu Ameanzisha Kurani Tukufu kwa aya hii hii: اَلۡحَمۡدُ لِلّٰهِ رَبِّ الۡعٰلَمِيۡنَ[4] . Na mahali mbalimbali ndani ya Kurani Tukufu Ameeleza waziwazi kabisa kuwa jambo hili siyo sahihi kuwa Manabii wa Mungu huwa wanakuja ndani ya taifa maalum au nchi maalum. Bali Mungu hakulisahau taifa lolote wala nchi yoyote. Ndani ya Kurani Tukufu mifano mbalimbali imetolewa kwa kueleza kuwa jinsi Mungu Alivyoendelea kuwapatia ulezi wa kimwili watu wa kila nchi kulingana na hali zao, ndivyo Alivyowapatia watu wa kila nchi na kila taifa malezi yao ya kiroho pia, kama Asemavyo sehemu fulani ndani ya Kurani Tukufu: وَاِنۡ مِّنۡ اُمَّةٍ اِلَّا خَلَا فِيۡهَا نَذِيۡرٌ[5] yaani hakuna taifa lolote ambamo ndani yake hakutumwa Nabii au Mjumbe yeyote.

---

[4] Sifa zote njema ni za Mungu, Mola wa walimwengu. Al-Faatiha, 1:2

[5] Faatir, 35:25

Basi, jambo hili linastahili kukubaliwa bila mjadala wowote kuwa Mungu Yule wa kweli na Mkamilifu Ambaye kumwamini ni faradhi ya kila mtu, Yu Mola wa walimwengu, na ulezi wake hauishii mpaka kwa taifa fulani maalum wala kwa zama maalum wala nchi maalum. Bali Yu Mola wa mataifa yote, Mola wa zama zote, Mola wa Mahali pote na Mola wa nchi zote. Yeye ndiye chemchemi ya baraka zote, na nguvu zote za kimwili na kiroho zinatokana kwake, vyote vilivyopo vinalelewa naye, na ndiye tegemeo la kila dhati.

Baraka za Mungu ni kwa wote, zinazojumuisha mataifa yote, nchi zote na zama zote. Hii imekuwa, ili taifa lolote lisipate nafasi ya kulalamika na lisiseme kuwa Mungu Aliyafanyia hisani mataifa fulani fulani tu lakini Hakutufanyia sisi; au taifa fulani lilipokea kitabu kutoka Kwake ili lipate mwongozo ndani yake lakini sisi hatukupatiwa, au katika zama fulani Yeye Alidhihiri na wahyi, ufunuo na miujiza, lakini katika zama zetu Akawa Amefichika. Hivyo, Yeye kwa kuonyesha baraka kwa wote Ameziondoa pingamizi zote na akaonyesha khulka zake zenye wasaa kiasi kwamba hakulinyima taifa lolote baraka zake za kimwili na kiroho wala hakuzifanya zama zozote kuwa ni za mkosi na bahati mbaya.

Hivyo, kwa kuwa hizo ndizo khulka za Mungu wetu,

basi inafaa kuwa sisi pia tuzifuate khulka hizo. Kwa hiyo, Enyi ndugu wananchi, kijitabu hiki kidogo ambacho jina lake ni *Ujumbe wa Amani,* kwa adabu kinafikishwa kwenu nyote, na kwa moyo wa kweli inaombwa kuwa yule Mungu Mweza Mwenyewe Awafunulieni ufunuo mioyoni mwenu, na awafungulieni siri ya huruma zetu mioyoni mwenu ili zawadi hii ya kirafiki msiione ni kwa lengo mahususi na shabaha fulani ya nafsi. Enyi wapendwa!! Mambo ya akhera mara nyingi huwa yamefichikana kwa watu wa kawaida, na siri za akhera hufunuliwa kwa wale tu wanaokufa kabla ya kufa kwao, lakini wema na ubaya wa dunia unaweza kujulikana kwa kila mwenye busara.

Jambo hili halikufichika kwa yeyote kuwa umoja ni jambo ambalo kwa njia yake mabalaa yasiyoweza kuondolewa kwa njia yoyote, na matatizo yasiyoweza kutatuliwa kwa tadbiri yoyote, hutatuliwa. Hivyo, haiwezekani mwenye akili ajinyime baraka hizo za umoja. Mabaniani na Waislamu ni mataifa mawili katika nchi hii. Ni muhali wazo hili kuwa wakati fulani, kwa mfano, Mabaniani wakijumuika watawatoa Waislamu katika nchi hii, au Waislamu wakiungana pamoja watawafukuza Mabaniani nchini. Bali hivi sasa Mabaniani na Waislamu wanakuwa kama chanda na pete; mmoja akifikiwa na

maangamio, na mwenzake pia atashiriki katika hayo. Na kama taifa moja kwa kiburi tu na majivuno yake ya kibinafsi litataka kulidunisha taifa jingine, basi hili lenyewe pia halitasalimika kudunishika. Na kama mojawapo la hayo mawili halitahurumia jirani, hilo lenyewe pia litajipatia hasara. Mtu yeyote miongoni mwa mataifa haya mawili anayefikiria maangamiao kwa ajili ya taifa lingine, mfano wake ni sawa na mtu yule anayelikata tawi lile lile alilojikalia. Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu nyinyi ni watu mlioelimika pia, sasa inafaa mwache chuki, mpate maendeleo katika upendo. Yafaa kuacha ubaridi na kujichagulia kufanya huruma, maana, hiyo ndiyo yaafikiana na busara yenu. Matatizo ya duniani ni safari ya jangwani inayofanywa katika kiangazi tena wakati jua linapokuwa kali. Basi, katika njia hii ngumu, kuna haja ya maji baridi ya umoja ya kuufanya baridi moto unaorindima na kuwaponyesha watu wasife kwa sababu ya kiu.

Katika wakati huu wa hatari, mimi mwandishi nawaiteni kwa ajili ya suluhu ambapo mataifa yote mawili yanahitaji sana suluhu. Mabalaa mbalimbali yanatokea duniani, matetemeko yanatokea, njaa inatanda na tauni pia haijaondoka. Na Aliyonihabarisha Mungu nayo ni haya haya kuwa kama dunia haitayaacha matendo yake mabaya na

haitatubia kufanya mambo maovu, basi dunia itakumbwa na mabalaa makubwa makubwa, na kabla balaa moja halijapita, balaa jingine litadhihiri. Mwishoni watu watasumbuka sana kuwa nini kinataka kutokea, na kwa kubanwa katikati ya misiba mingi watu watakuwa kama wendawazimu. Hivyo, Enyi ndugu wananchi, zindukeni kabla hazijawadia siku hizo kutokea. Inatakiwa Mabaniani na Waislamu wafanye suluhu baina yao. Taifa lenye uonevu ambao ni kizuizi cha suluhu, na liachane kabisa na uonevu huu, waila dhambi za uadui wote baina yao zitakuwa juu ya shingo ya taifa hilo hilo.

Kama mtu aseme kuwa yawezaje suluhu kupatikana ilhali hitilafu za dini ni kikwazo cha suluhu kinachoendelea kuchochea mfarakano ndani ya mioyo siku hadi siku.

Mimi nikilijibu nitasema kuwa kwa kweli hitilafu ya kidini ni jina tu la ile hitilafu ambayo msingi wake, kwa pande zote mbili, ni juu ya akili, adili na mambo yanayoshuhudia. La sivyo, mtu amejaliwa akili ili ashikamane na ule upande usio kinyume cha akili na adili, wala usiwe kinyume na mambo yanayohisiwa na kushuhudiwa. Hitilafu ndogo ndogo haziwezi kuzuia suluhu, bali hitilafu ile tu inazuia suluhu ambayo kwa sababu yake Mtume aliyekubaliwa na watu na kitabu cha ufunuo kilichokubaliwa nao vishambuliwe kwa

kudharau na kukadhibisha. Isitoshe, ni jambo la furaha kubwa kwa wapendao amani kwamba mafundisho yoyote yaliyo ndani ya Islam yote hayo yanapatikana ndani ya sehemu hii au ile ya mafundisho ya Veda. Kwa mfano, dhehebu changa la Aria Samaji linafundisha kuwa baada ya ma-Veda ufunuo wa Mungu umepigwa muhuri; lakini *ma-Autar* walioendelea kuzaliwa ndani ya dini ya Kibaniani katika nyakati mbalimbali ambao mamilioni ya wafuasi wao wanaopatikana nchini humu, wamekwisha vunjilia mbali muhuri huo kwa madai yao ya ufunuo. Kwa mfano, *Autari* mmoja mkubwa anayekubaliwa katika nchi hii na huko Bengal kwa heshima kubwa na adhama, jina lake Sri Krishna, anadai kuwa alipokea ufunuo, na wafuasi wake si tu wanamwamini kuwa alifunuliwa ufunuo, bali wanamwamini kuwa yeye ni *Parmeshar* (mungu). Hakuna shaka ndani yake kuwa Sri Krishna alikuwa Nabii na *Autari* wa zama zake, na Mungu Alikuwa anaongea naye.

Vivyo hivyo katika zama hizi za mwisho yuko Bwana Baba Nanak kutoka ndani ya kaumu ya Mabaniani, ambaye umaarufu wa utawa wake unafahamika sana kwa kila mmoja nchini humu, ambaye hapa nchini wafuasi wake ndio wanaoitwa Makalasinga, idadi ya siyo chini ya milioni mbili. Baba Sahib ndani ya *ma-*

*Janam Sakhi* na *Granth* anadai waziwazi kupokea ufunuo, hata kwamba ndani ya Janam Sakhi yake moja anaandika kuwa mimi nimefunuliwa na Mungu kwamba dini ya Islam ni ya kweli. Kwa sababu hiyo akafanya hija. Na akashikamana na itikadi zote za Kiislamu. Na bila shaka jambo hili linathibitika kuwa alizionyesha pia karama na ishara. Na hakuna shaka ndani ya jambo hili kuwa Baba Nanak alikuwa mtu mwema na mteule, na alikuwa miongoni mwa watu wale ambao Mungu Mtukufu Mwenye enzi Anawanywesha sharubati ya mapenzi yake. Yeye alizaliwa ndani ya Mabaniani ili kutoa tu ushahidi kwamba Islam ndiyo kutoka kwa Mungu. Mtu yule anayeyaona masalio yake yaliyomo ndani ya *Dera Nanak*, ambamo ametoa kwa nguvu sana ushahidi wa *kalima* لَآ اِلٰهَ اِلَّا اللهُ مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللهِ na kisha ayashuhudia masalio yake yaliyopo pale paitwapo Guru Harsahae, wilayani Ferozpur, ambamo nakala moja ya Kurani Tukufu pia imo, yeye mtu huyo anawezaje kuwa na shaka ndani ya jambo hili kuwa Bwana Baba Nanak kwa moyo wake uliotakasika na kwa asili yake iliyotakata na kwa juhudi zake njema aliishaigundua siri ile iliyokuwa imefichikana kwa Mapandati wa kidhahiri. Naye kwa kudai kupokea ufunuo na kwa kuonyesha ishara na karama kutoka kwa Mwenyezi Mungu akaivunjilia mbali itikadi hii kuwa hakuna

ufunuo baada ya Veda wala hakuna ishara zidhihirikazo. Bila shaka dhati ya Bwana Baba Nanak kwa ajili ya Mabaniani ilikuwa ni rehema kutoka kwa Mungu, na fahamuni kuwa yeye kwa ajili ya dini ya Kibaniani alikuwa *Autaar* — walii — wa mwisho aliyetaka kuiondoa chuki iliyokuwemo ndani ya mioyo ya Mabaniani dhidi ya Islam. Lakini ni bahati mbaya pia ya nchi hii kuwa dini ya Kibaniani haikujinufaisha chochote na mafundisho ya Bwana Baba Nanak, bali Mapandati wakamsumbua kwamba kwa nini kila mahali anaisifu Islam. Yeye alikuja kuleta suluhu baina ya dini ya Kibaniani na Islam. Lakini ni masikitiko kuwa hakuna aliyejali mafundisho yake. Kama kwa dhati yake na kwa mafundisho yake wangenufaika kidogo, leo Mabaniani na Waislamu wangekuwa kitu kimoja. Hae! Ole wao!! Fikara hii tu inaliza kuwa mja mwema kama huyo alikuja duniani na akaondoka pia, lakini watu wasiojua hawakupata mwanga hata kidogo kutokana na nuru yake.

Kwa vyovyote, yeye akaondoka akiishathibitisha kuwa wahyi wa Mungu na ufunuo wake haukatiki kamwe, na ishara za Mungu zinaendelea kudhihirika sikuzote kwa njia ya wateule wake. Na akaondoka akiishatoa ushahidi kuwa uadui wa Islam ni uadui wa nuru.

Mimi nami nina tajiriba kuwa wahyi wa Mungu na ufunuo wa Mungu haukukatizwa kabisa katika zama hizi, bali kama Mungu Alivyokuwa Anaongea hapo awali ndivyo Anavyoongea hata sasa pia, na kama Alivyokuwa Anasikia hapo awali, ndivyo Asikiavyo sasa pia. Siyo kuwa sifa zake za zamani sasa zimetoweka. Mimi tangu karibu miaka thelathini naendelea kupata heshima ya maongezi na Mungu. Amedhihirisha mamia ya ishara kwa mikono yangu zilizoshuhudiwa na maelfu ya watu na ambazo zimechapishwa ndani ya vitabu na magazeti, na hakuna taifa lolote lisilokuwa shahidi wa ishara hii au ile.

Sasa pamoja na mfululizo wa shuhuda zote hizo, mafundisho haya ya Aria Samaj yanayonasibishwa kwenye Veda, yawezeje kukubalika kwamba — wanasemavyo — silsila yote ya maongezi ya Mungu na ufunuo wake imeishia kwenye Veda, kisha baada ya hapo mategemeo ni juu ya visa tu. Na kwa sababu ya itikadi yao hii wanasema kuwa mbali na Veda vitabu vingine vyote vilivyopo duniani vya ufunuo wa Mungu, vyote hivyo, Mungu Apishe mbali, ni uzushi wa wanadamu, ilhali vitabu hivyo vinajithibitishia ukweli wao zaidi sana kuliko Veda, na Mkono wa msaada na nusura za Mungu uko pamoja navyo na ishara zilizo zaidi ya kawaida za Mungu zinatoa ushahidi wa ukweli wao. Sasa kwa nini Veda ndiyo

iwe maneno ya Mungu lakini vitabu hivyo vingine visiwe maneno ya Mungu? Na kwa vile dhati ya Mungu ni yenye kina kirefu zaidi na imefichikana sana, hivyo akili pia inataka kwa ajili ya kuthibitisha uwepo wake Asitosheke kwa kitabu kimoja tu, bali Akiwateua Manabii katika nchi mbalimbali, Aongee nao na kuwafunulia ufunuo wake ili mwanadamu mdhaifu anayeweza kuingiwa na shaka kwa haraka asikose nafasi ya kukubali.

Na akili timamu haiko tayari kukubali kuwa Mungu Yule Ambaye ni Mungu wa dunia, Anayeangaza magharibi na mashariki kwa jua lake, na kwa mvua yake huinywesheleza kila nchi wakati wa kila haja, Yeye, Mungu Apishe mbali, katika malezi ya kiroho Yu bahili na mwenye moyo finyu hata kwamba kwa kudumu aipenda nchi moja, taifa moja na lugha moja tu, nami siwezi kuelewa kuwa ni mantiki ya aina gani hii na falsafa ipi kuwa *Permesher* anaweza kuelewa dua na maombi ya kila mmoja katika lugha yake na haonyeshi chuki yoyote, lakini Anachukia sana kuteremsha nyoyoni ufunuo mbali na lugha ya Sanskiriti. Falsafa hii au maarifa ya Veda ni kama fumbo ambalo mpaka leo hakuna mwanadamu aliyeweza kulifumbua.

Mimi nafahamu Veda imeepukana na kuchapa kwenye ukurasa wake wowote mafundisho ambayo

siyo tu kinyume cha akili, bali yanatia katika dhati takatifu ya Mungu doa la ubahili na kupendelea upande mmoja. Bali ukweli ni huu kuwa muda mrefu unapokipitia kitabu cha ufunuo, wafuasi wake kwa sababu ya kutojua na pia kwa sababu ya matamanio ya nafsi, kwa kusahau au kwa makusudi huongezea maelezo ya pembeni na kwa vile wanaotia nyongeza huwa ni watu wenye mawazo mbalimbali, hivyo basi kutoka dini moja huzalika mamia ya madhehebu mengine.

Na hili ni jambo la ajabu kuwa kama vile jamaa Waaria wanavyoitakidi kuwa silsila ya ufunuo wa Mungu imewekewa mipaka kwa ajili ya koo za Waaria na nchi yao India tu, daima lugha ya ki-Veda ya Kisanskriti ndiyo imekuwa maalum kwa ajili ya ufunuo wa Mungu, na hiyo ndiyo lugha ya Mungu, ndivyo yalivyo mawazo ya Wayahudi kuhusiana na ukoo wao na vitabu vyao. Hao nao wanafikiri kuwa lugha hasa ya Mungu ni Kiebrania na silsila ya ufunuo ilikuwa na mipaka mpaka kwa Bani Israeli na nchi yao tu, na mtu anayedai unabii ilhali yuko nje ya ukoo wao na lugha yao, Mungu Apishe mbali, wao wanamchukulia kuwa ni mtu mwongo.

Sasa, je kulingana huku si jambo la kushangaza kuwa mataifa haya yote mawili ndani ya maelezo yao yametoa fikara ya aina moja? Vivyo hivyo, duniani

kuna makundi mengine mengi pia yanayoshikamana na fikara hii hii, kama vile Maparsi wanaosema kuwa msingi wa dini yao ni tangu mamilioni ya miaka kabla ya Veda. Hii inaonyesha kuwa wazo hili (kuwa nchi yao, ukoo na lugha yao tu ndiyo iliyoteuliwa kwa kudumu kwa wahyi na ufunuo wa Mungu) limezalika tu kwa sababu ya upendelevu na uchache wa ujuzi. Kwa vile zama zile zimepita duniani ambapo taifa moja halikuwa na habari za taifa lingine na nchi moja haikujua uwepo wa nchi nyingine, hivyo kutokana na kosa hili kila taifa lililopata kitabu kutoka kwa Mungu, au akaja katika taifa hilo Nabii au Mjumbe wa Allah, taifa hilo likafikiria kuwa mwongozo wowote uliotakiwa uje kutoka kwa Mwenyezi Mungu ni huu huu tu, na Kitabu cha Mungu umepewa ukoo wao na nchi yao tu, na watu wote wengine waliobaki wamekosa bahati hii.

Mawazo haya yameiletea dunia hasara kubwa, na kwa kweli mbegu za chuki na bughudha zilizoendelea kukua baina ya watu ni kutokana na mawazo haya haya tu. Kwa muda fulani taifa moja lilikuwa nyuma ya pazia kwa taifa jingine na nchi moja ilikuwa imefichikana na nchi nyingine kiasi kwamba maulamaa wa India walikuwa wakidhania kuwa nyuma ya milima ya Himalaya hakuna watu kabisa.

Kisha wakati Mungu Alipoondoa pazia katikati, na

ujuzi wa watu ukapanuka kiasi fulani kuhusiana na ardhi kukaliwa na watu, hizo zilikuwa ni zama ambapo zile sifa teule walizokuwa wamezibuni watu nyonyoni mwao na kuziingiza katika itikadi zao, kuhusu vitabu vyao vya ufunuo na Marishii na Mitume wao, na zikaimarika katika mioyo yao sana kiasi kwamba zisiweze kufutika, na kila kaumu ikafikiria kuwa siku zote makao makuu ya Mungu yamekuwa ndani ya nchi yao. Na kwa vile katika siku hizo mataifa mengi yalitawaliwa na tabia za kinyama, na mpinzani wa desturi yao ya zamani akajibiwa kwa upanga, hivyo nani alithubutu kuwasuluhisha kwa kupoza jazba za majisifu ya kila taifa! Gautama Budha alidhamiria kufanya suluhu baina yao. Yeye hakuamini kuwa kila kitu ni Veda tu, hakuna kitu baada yake. Yeye hakukubali uteule wa taifa fulani na nchi na ukoo, yaani haikuwa imani yake kuwa yote yanaishia kwa Veda tu, lugha hii tu, nchi hii hii tu, na ni *Mabarahman* hawa hawa tu waliosajiliwa kwa kudumu mahakamani mwa *Parmesher* kwa ajili ya kupata ufunuo. Basi yeye alipata mateso makubwa kutokana na hitilafu hizi. Yeye akaitwa kuwa hamwamini Mungu wala hana dini, kama ambavyo wahakiki wote wa Ulaya na Amerika wa siku hizi ambao hawakubali Uungu wa Hadhrat Isa, na mioyo yao haiamini kuwa Mungu pia Anaweza kuwambwa

msalabani, wanafikiriwa na Mapadre kuwa *daharia*, yaani wasiomwamini Mungu.

Basi, Budha pia akahesabiwa kuwa *daharia* wa aina hii. Na kama ilivyo desturi za wapinzani wenye shari, akazushiwa tuhuma nyingi ili kuzalisha chuki ndani ya watu wa kawaida. Mwishoni matokeo yakawa kuwa Budha akafukuzwa kutoka India iliyokuwa nchi yake alikozaliwa, na mpaka sasa Mabaniani wanaiangalia kwa chuki na dharau sana dini ya Kibudha na ufaulu wake. Lakini kwa muafaka wa kauli ya Hadhrat Isa[as], "Nabii havunjiwi heshima ila katika nchi yake", Budha akihamia nchi nyingine alipata mafanikio makubwa. Kama inavyoelezwa, theluthi ya dunia imejaa dini ya Kibudha, na kwa wingi wa wafuasi wake makao makuu yake ni China na Japan, ingawa imeshaenea hadi kusini mwa Urusi na Amerika pia.

Sasa tukirudia maelezo yetu tunaandika kuwa katika zama zile ambapo dini moja haikuwa na habari ya dini nyingine, katika hali hii ya kutojuana ilikuwa hakuna budi kila taifa liishie kwa dini yake na kitabu chake tu. Lakini matokeo ya kuishia huku yakawa kuwa nchi moja ilipoijua nchi nyingine na watu wa nchi mbalimbali walipopata taarifa ya dini za nchi zingine, hapo ikawa vigumu kwao kwamba dini ya nchi moja iwaze kuisadikisha dini ya nchi nyingine. Maana, kwa

kila dini, ziliisha andaliwa sifa maalum na sifa bora bora zilizotiwa chumvi kishairi, kuziondoa hizo haikuwa kazi rahisi. Hivyo, mfuasi wa kila dini akawa amepania kuikadhibisha dini nyingine. Dini ya *Zand* na *Avista* – Zoroaster – ikadai kwamba hakuna yeyote aliye sawa nasi. Na silsila ya unabii waliiwekea mpaka ukoo wao, na wakaielezea historia ya dini yao kuwa ina muda mrefu sana sana kiasi cha kuwafanya waelezaji wa historia ya Veda wanaona haya mbele yao.

Huku nako dini ya Kiebrania nayo ikatia fora kwa kuyafanya makao makuu ya Mungu kuwa nchi ya Shamu, na daima watawa wa ukoo wao tu ndio waliostahili watumwe kwa ajili ya kuleta urekibisho nchini. Lakini kwa amri usuluhishi huo ulibakia kwa wana wa Israeli tu, na ukoo wao uliteuliwa kupata ufunuo na wahyi, na mwingine yeyote aliyedai alichukuliwa kuwa ni mwongo.

Kadhalika, katika India yalienea mawazo kabisa kama hayo na yaliyoene baina ya Waisraeli. Na kwa mujibu wa itikadi zao, *Parmeshar* ni mfalme tu wa nchi ya India, na ni mfalme asiye na habari ya nchi zingine. Na bila dalili yoyote inaaminiwa kuwa tangu awepo *Parmeshar* duniani, yeye amependezwa na hali ya hewa ya India, kamwe hataki kuzitembelea nchi zingine akawajulie hali ya wale maskini ambao

aliwasahau baada ya kuwaumba.

Marafiki! Fikirini, kwa ajili ya Mungu mkaangalie kuwa je itikadi hizi ndizo ambazo tabia ya asili ya mtu inaweza kuzikubali, au akili yoyote inaweza kuzipokea? Siwezi kufahamu kuwa hii ni akili ya aina gani kwamba upande mmoja kumkubali Mungu kuwa ni Mungu wa dunia nzima kisha kusema pia kwa kinywa hicho hicho kuwa Yeye amejiondoa kuchukua jukumu la malezi ya dunia nzima. Analitazama taifa moja tu mahususi, na nchi moja tu maalumu, kwa jicho la huruma. Enyi wenye akili!! Fanyeni adili wenyewe kuwa je ndani ya kanuni za kimwili za Mungu mna ushahidi wake wowote? Basi kwa nini kanuni yake ya kiroho iwe na msingi wa upendeleo kama huo.

Na kama akili itumiwe, uzuri au ubaya wa kila kazi huweza kujulikana kutokana na matokeo yake. Basi, mimi sina haja ya kueleza kwamba kuwavunjia heshima ya Manabii watukufu wa Mungu na kuwatukana, ambao mamilioni ya watu wa kila tabaka wameshaingia chini ya ufuasi na utii wao, natija yake itakuwaje na hatimaye matokeo yake yatakuwa nini, maana hakuna hata taifa moja ambalo halijawahi kushuhudia kiasi chochote matokeo ya aina hii.

Enyi wapendwa!! Tajiriba ya zamani na majaribio ya mara kwa mara vimethibitisha jambo hili kuwa kuwadharau manabii na wajumbe wa mataifa mbalimbali na kuwatukana ni sumu ambayo siyo tu kuwa mwishoni huuangamiza mwili, bali ikihilikisha roho huangamiza dini na dunia zote mbili pia. Nchi ile haiwezi kupata utulivu ambayo wananchi wake wanashughulikia kutoa aibu na kuwavunjia heshima viongozi wa dini wa wenzao. Na mataifa yale hayawezi kupata kabisa umoja wa kweli ambayo kati yao taifa mojawapo au yote mawili yanaendelea kumtusi Nabii au *Rishii* na *Autar* wa wenzao. Nani hapandishiwi jazba kwa kusikia kudharauliwa kwa Nabii au Mwongozi wake. Hususan Waislamu ni watu ambao ingawa hawamchukulii Nabii wao kuwa Mungu au mwana wa Mungu, lakini wanamwamini Mtume s.a.w. kuwa mbora wa wateule wote waliozaliwa kutoka tumboni mwa mama. Hivyo, kufanya suluhu na Mwislamu wa kweli haiyumkiniki kwa hali yoyote isipokuwa tu kuwa maongezi yanapofanyika kuhusu Mtume Mtukufu[saw] basi Mtume atajwe kwa heshima na kwa maneno mazuri.

Na sisi hatutumii lugha chafu kuhusu Manabii wa mataifa mengine. Bali tunayo itakidi hii hii kuwa Manabii wote waliokuja duniani ndani ya mataifa mbalimbali na mamilioni ya watu wakawaamini, na

sehemu fulani ya dunia imeingiwa na upendo wao na adhama yao, na muda mrefu umepita juu ya upendo huu na itikadi hii, basi hii inatosha kuwa dalili ya ukweli wao. Kwani, kama wasingekuwa wametoka kwa Mungu, kukubaliwa huku kusingeenea ndani ya mioyo ya mamilioni ya watu. Mungu kamwe Hawapi wengine heshima ya waja wake waliokubaliwa naye. Na kama mwongo yeyote akitaka kujikalia kiti chao, mtu huyo huangamia haraka na kuangamizwa.

Kwa sababu hiyo tunaamini kuwa Veda pia imetoka kwa Mungu na *Marishii* wake tunawatambua kuwa watawa na watakatifu, ingawa tunaona kuwa mafundisho ya Veda hayakuweza kulifanya dhehebu lolote limwabudu Mungu kikamilifu, wala yasingeweza kufanya hivyo. Na wale watu wanaopatikana ndani ya nchi hii wanaoabudu masanamu au moto au jua au mto Ganges au wanayaabudu maelfu ya miungu au watu wa dini ya *Jaini* au dini ya *Shakti*, hao wote wanazinasibisha dini zao kwenye Veda tu. Na Veda ni kitabu kinachohitaji maelezo, hivyo madhehebu yote yanatoa matilaba yao kutoka humo humo. Hata hivyo, kwa mujibu wa mafundisho ya Mungu tuna itikadi madhubuti kuwa Veda haikutungwa na mtu. Ndani ya utungo wa mtu huwa hamna nguvu ya kuwavutia mamilioni ya watu upande wake na kisha kuimarisha silsila ya kudumu.

Ingawa hatukusoma popote ndani ya Veda juu ya kuyaabudu mawe, lakini bila shaka Veda imejaa ibada ya Moto, Hewa, Maji, Mwezi, Jua na vinginevyo, na katika aya yoyote haikukatazwa kuviabudu vitu hivyo. Sasa, nani atatoa uamuzi kuwa madhehebu mengine yote ya kale ya Kibaniani ni ya uongo na dhehebu jipya la Waaria ndilo la kweli. Na wale watu wanaoviabudu vitu hivyo kwa kutumia vielelezo vya Veda, wana dalili hii madhubuti mikononi mwao kuwa kuna maelezo ya wazi ndani ya Veda juu ya kuviabudu vitu hivyo na hakuna katazo mahali popote. Na kusema kuwa haya yote ni majina ya *Permeshar*, bado hili ni dai tu ambalo mpaka sasa halijaamuliwa barabara. Na kama ingeisha amuliwa tayari, basi haionekani sababu yoyote kuwa Mapandit wakubwa wakubwa wa Banaras na miji mingine wasingekubali itikadi za Waariya. Juu ya juhudi za miaka thelathini au thelathini na mitano, ni Mabaniani wachache sana waliojiunga na dhehebu la *Kiaria*. Na kwa kulinganisha na Sanatan Dharm na madhehebu mengine ya Kibaniani, wafuasi wa dhehebu la Kiaria ni wachache sana kana kwamba si chochote, na hawana athari kubwa juu ya madhehebu mengine ya Kibaniani. Vivyo hivyo, mafundisho ya *Neyoga,* yanayonasibishwa kwa Veda, pia ni jambo ambalo ghera ya kibinadamu na uungwana

haulikubali. Lakini, kama nilivyobainisha sasa hivi, hatuwezi kukubali kuwa haya kwa kweli ndiyo mafundisho ya Veda, bali nia yetu njema kwa nguvu sana inatuelekeza kwenye jambo hili kuwa mafundisho kama haya yalinasibishwa baadaye kwa kitabu cha Veda kwa makusudio fulani ya nafsi. Na kwa vile maelfu ya miaka imepita juu ya Veda, hivyo inawezekana kuwa katika zama mbalimbali baadhi ya watoaji maelezo ya Veda wakapunguza na kuongeza kwa namna mbalimbali. Basi, dalili hii moja inatosha kwetu kwa ukweli wa Veda kuwa mamilioni ya waumini wa India tangu maelfu ya miaka waliendelea kuamini kuwa Veda ni maneno ya Mungu, na haiyumkiniki kuwa heshima hii yapewe maneno ambayo ni maneno ya mzushi.

Na kisha juu ya matatizo haya yote, kwa kumwogopa Mungu, tunapoichukua Veda kuwa ni maneno ya Mungu na makosa yoyote yaliyamo ndani ya mafundisho yake, tukiyaamini kuwa ni makosa ya watoaji maelezo tu wa Veda, kwa nini Kurani Tukufu inashambuliwa kinyama iliyojaa Umoja wa Mungu kutoka mwanzo mpaka mwisho na mahali popote haina mafundisho ya kuabudu jua na mwezi na kadhalika, bali kwa maneno ya wazi kabisa imesema:

لَا تَسْجُدُوْا لِلشَّمْسِ وَلَا لِلْقَمَرِ وَاسْجُدُوْا لِلّٰهِ الَّذِيْ خَلَقَهُنَّ [6]

Yaani, msiabudu jua wala mwezi, wala kiumbe kingine, na mwabuduni Aliyewaumbeni. Isitoshe, Kurani Tukufu inao ushahidi wa ishara za kale na ishara mpya, na ni kioo cha kuonyesha dhati ya Mungu. Kwa nini hatutendewi jinsi tunavyowatendea Waaria, na kwa nini mbegu za uadui na chuki zinapandwa nchini. Je, yatarajiwa kuwa matokeo yake yatakuwa mazuri? Je, ni tendo jema kuwa mtu anayekupa maua atupiwe mawe, na yule anayekupa maziwa amwagiwe mkojo?

Kama Mabaniani na Waariya wako tayari kwa suluhu ya aina hii kuwa wao wamtambue Mtume wetu s.a.w. kuwa ni Nabii wa kweli wa Mungu na tangu sasa waache kumfedhehesha na kumkadhibisha, basi mimi ni mtu wa kwanza kuwa tayari kutia saini kwenye makubaliano haya kuwa sisi wafuasi wa Jumuiya ya Ahmadiyya daima tutakuwa wasadikishaji wa Veda, na tutaitaja Veda na Marishii wake kwa heshima na upendo. Na kama hatutafanya hivi, basi kiasi kikubwa cha fedha ya fidia isiyopungua rupia laki tatu tutawapatia Mabaniani. Na kama Mabaniani wanataka kwa moyo mkunjufu kufanya suluhu nasi, basi wao pia wanatakiwa watie saini kwenye

[6] Haa Miim As-Sajda, 41:38

makubaliano ya maandishi ya aina hiyo hiyo. Na madhumuni yake itakuwa ni kuwa sisi tunauamini Utume na Unabii wa Hadhrat Muhammad Mustafa[saw] na kwamba tunamkubali Mtume[saw] kuwa Nabii na Mjumbe mkweli na tangu sasa tutamtaja kwa heshima na adabu kama ilivyo hali ya mwaminio. Na tusipofanya hivyo, basi tutamtolea Kiongozi wa Jumuiya ya Ahmadiyya kiwango kikubwa cha fidia kisichopungua rupia laki tatu. Ikumbukwe kuwa Jumuiya yetu ya Ahmadiyya ina wafuasi wasiopungua laki nne, hivyo kuchanga rupia laki tatu si kitu kikubwa kwa ajili ya kazi kubwa ya aina hii. Na wale watu ambao bado wako nje ya Jumuiya yetu, hao kwa kweli ni wale wenye tabia na mawazo yaliyoparaganyika. Hao hawako chini ya kiongozi ambaye wanawajibika kumtii, hivyo siwezi kuongea chochote juu yao. Kwa hivi sasa mimi pia wananichukulia kuwa ni kafiri na dajali. Lakini ninatumaini kuwa ndugu Mabaniani watakapofanya mapatano ya namna hii nami, watu hao pia hawatatenda ovyo kwa kutumia maneno mabaya kuhusiana na kitabu cha taifa lililostaarabika kama hili na Marishii wao wasababishe Mtume Mtukufu[saw] atukanwe. Kwa kweli matusi ya aina hii yatahesabiwa kutoka kwa wale tu watakaofanya utundu huo. Na kwa vile kitendo cha aina hii ni kinyume cha haya na

uungwana, hivyo mimi situmaini kuwa baada ya mapatano haya watu hao watafungua midomo yao. Lakini itakuwa ni lazima kuwa ili kuyapatia nguvu maandishi ya mapatano, watu elfu kumi wenye busara wa kila upande watie saini juu ya mapatano hayo.

Wapendwa!! Hakuna kitu kilicho kama suluhu. Njooni, basi, kwa njia ya mapatano hayo tuwe kitu kimoja na tuwe taifa moja. Nyinyi wenyewe mnashuhudia kuwa kutokana na kukadhibishana, mvurugano kiasi gani umetokea, na nchi yapata hasara kiasi gani. Njooni, sasa, mkajaribu hii pia kwamba katika kusadikishana kuna baraka kiasi gani. Njia bora zaidi ya suluhu ni hii hii, waila kufanya suluhu kwa njia nyingine ni sawa tu na jipu moja safi linalong'aa liachwe katika hali hiyo hiyo na kufurahia mng'ao wake huo, ilhali ndani yake mna usaha uliooza unaonuka.

Mimi sina lengo lolote kuelezea habari hizi hapa kuwa ule unafiki na ufisadi unaoendelea kuzidi baina ya Mabaniani na Waislamu siku hizi, sababu zake haziishii tu kwenye hitilafu za kidini pekee, bali sababu zake ni makusudio mengine yanayohusikana na dunia na mambo yake. Kwa mfano, Mabaniani tangu mwanzo walitamani wapate kuingilia mambo ya Serikali na ya nchi, au kwa uchache waombwe kutoa rai zao kuhusu kuendesha mambo ya nchi, na

Serikali iyasikilize malalamiko yao kwa makini, na vyeo vikubwa vikubwa vya Serikali wanavyopewa Waingereza nao pia wapewe. Kosa lililofanywa na Waislamu ni kuwa wao hawakushirikiana na Mabaniani katika juhudi zao hizi, na wakafikiri kuwa sisi tuko wachache katika idadi, na wakafikiria pia kwamba kama kuna faida yoyote ya juhudi hizi, basi ni kwa ajili ya Mabaniani tu, siyo kwa ajili ya Waislamu, kwa hiyo siyo tu kuwa hawakushiriki nao, bali wakapinga juhudi za Mabaniani kwa kuwazibia njia na kwa sababu hii uhasama ukaongezeka zaidi.

Mimi ninakubali kuwa kwa sababu hizi pia uadui wenyewe umenyunyiziwa chumvi, lakini sitakubali kuwa hizi hizi ndizo sababu, wala siafikiani na rai za wale wanaosema kuwa uadui na unafiki baina ya Mabaniani na Waislamu, sababu zake siyo magomvi ya kidini, magomvi yao ya kweli ni ya kisiasa.

Kila mtu anaweza kuelewa kwa urahisi kwamba kwa nini Waislamu wanaogopa kushirikiana na Mabaniani katika kudai haki zao, na kwa nini mpaka leo wameendelea kukataa kujiunga na chama chao cha Congress? Na kwa nini baada ya kuhisi rai za Mabaniani kuwa sahihi mwishowe wakafuata hatua yao, lakini wakiwa mbali na hao, na wakaunda Chama cha Kiislamu, lakini hawakukubali kushirikiana nao.

Enyi mabwana!! Sababu yake kwa kweli ni dini tu, hakuna nyingine ghairi ya hii. Kama leo Mabaniani hao hao wakiisoma *Kalima* takatifu لا اله الا الله محمّد رسول الله waje wakumbatiane na Waislamu, au kama Waislamu wakiwa Mabaniani waanze kufanya ibada ya moto, hewa, na vinginevyo sawa na amri ya Veda, na waiache Islam, basi magomvi yote mnayoyaita ni ya kisiasa yatafutika mara moja kana kwamba hayakuwepo asilani.

Basi, ni dhahiri kuwa mzizi wa bughudha na chuki yote kwa kweli ni hitilafu ya dini. Kila mara hitilafu hiyo ya dini ilipofikia kilele tangu zamani, ilikuwa inatiririsha damu. Enyi Waislamu, kwa sababu ya tofauti ya dini, Mabaniani wanawachukulieni nyinyi kuwa taifa tofauti na wao, na kwa sababu hiyo hiyo nyinyi nanyi mnawafikiria hawa kuwa taifa lingine, hivyo bila kuondoa sababu hiyo iweje upatikane usafi wa kweli wa moyo baina yenu na yao? Naam, inawezekana kusuhubiana kupatikana kiunafiki kwa siku chache. Lakini ule usafi wa moyo unaopaswa kuitwa usafi wa kweli, utazalika katika hali ambapo nyinyi mtaikubali kwa moyo wa kweli kuwa Veda na Marishii wa Veda wametoka kwa Mungu. Vivyo hivyo Mabaniani pia wakiondokana na ubahili wao wausadikishe Unabii wa Mtume wetu[saw]. Kumbukeni na kumbukeni, sawa sawa, kuwa kati ya nyinyi na

Mabaniani kanuni ya kuleta suluhu ya kweli ni kanuni hii hii moja tu, na haya tu ndiyo maji ambayo yatazìosha takataka zote. Na kama siku zimefika kwamba mataifa haya mawili yaliyotengana yaungane, basi Mungu Atafungua mioyo yao pia kwa ajili ya jambo hili ambalo kwalo Ameshafungua moyo wetu.

Lakini pamoja na hayo itawalazimu kuwatendea Mabaniani kwa huruma ya kweli. Kuwatendea wema na upole kuwe mazoea yenu. Na mjiepushe na vitendo vitakavyowaumiza, lakini vitendo hivyo ndani ya dini yetu visiwe katika wajibu wala faradhi za dini yetu. Hivyo, kama Mabaniani kwa moyo wa ukweli wakubali Mtume wetu[saw] kuwa ni Nabii mkweli na wamwamini, basi mfarakano huu unaotokana na ng'ombe nao pia uondolewe. Kitu tunachokiona ni halali, hatuwajibiki lazima tukitumie. Kuna vitu vingi sana ambavyo tunajua kuwa ni halali lakini kamwe hatujavitumia. Watendeeni wema na hisani. Agizo mojawapo la dini yetu ni kumtambua Mungu Mmoja Asiye na mshirika. Basi kukiacha kitu kisicho lazima kwa ajili ya kazi ya lazima na ya manufaa siyo kinyume cha sheria ya Mungu. Kujua kitu fulani ni halali ni jambo jingine na kukitumia ni jambo jingine. Dini ndiyo kujiepusha na makatazo ya Mungu na kukimbilia njia za radhi yake, kuwafanyia wema na huruma viumbe

vyake wote, na kuwaamini Manabii na Mitume wote watakatifu waliokuja kutoka kwa Mungu katika nyakati zao kuwa Nabii na Muslih na kutotofautisha baina yao, na kumtendea kila mtu wema, ndio kiini cha dini yetu. Lakini wale watu ambao bila haki, bila kumwogopa Mungu, wanamtaja Mtume wetu mtukufu Muhammad Mustafa[saw] kwa maneno mabaya na wanamtuhumu kwa tuhuma chafu, wala hawaachi kutumia midomo michafu, vipi tufanye suluhu nao. Mimi ninasema kweli kabisa kuwa tunaweza kufanya suluhu na nyoka wa jangwani na mbwa mwito wa nyikani, lakini hatuwezi kufanya suluhu na watu ambao wanamfanyia mashambulizi machafu Nabii wetu mpendwa ambaye twampenda kuliko uhai wetu na mama na baba yetu. Mungu Atufishe ndani ya Uislamu. Sisi hatutaki kutenda matendo yatakayosababisha imani zetu kupotea.

Mimi hivi sasa sitaki kulilaumu bila sababu taifa lolote maalum, wala kuumiza moyo wa yeyote, bali kwa masikitiko makubwa nimelazimika kusema kuwa Islam ilikuwa dini takatifu na ya suluhu, ambayo haikuwahi kumshambulia kiongozi wa taifa lolote lile. Na Kurani Tukufu ni kitabu kinachopasa kuheshimiwa ambacho kimeweka msingi wa suluhu baina ya mataifa na kimemkubali Nabii wa kila taifa. Na duniani kote Kurani Tukufu tu inayo fahari hii

ambayo kuhusu dunia imetufundisha kwamba:

لَا نُفَرِّقُ بَيْنَ اَحَدٍ مِّنْهُمْ ۖ وَنَحْنُ لَهٗ مُسْلِمُوْنَ ○[7]

Yaani, Enyi Waislamu! Semeni kuwa sisi tunawaamini Manabii wote waliotumwa duniani na hatutofautishi baina yao kuwa baadhi yao tuwaamini na baadhi yao tuwakatae. Na kama kuna kitabu kingine cha ufunuo cha kuleta suluhu kama hiyo basi tajeni jina lake. Kurani Tukufu haikuhusisha rehema ya Mungu iliyo kwa wote, kwa ukoo wowote maalum. Manabii wote wa nyumba ya Israeli kama Yakubu[as] na Isihaka[as] na Musa[as] na Daudi[as] na Isa[as], Unabii wa wote hao imeukubali. Na Nabii wa kila taifa awe aliishi katika India au Uajemi, haikumwita yeyote kuwa mjanja na mwongo, bali imesema wazi kuwa katika kila taifa na ndani ya kila kijiji manabii walifika na wakaweka msingi wa amani kwa mataifa yote. Lakini ni masikitiko kuwa Nabii huyu wa amani, kila taifa linamtukana na kumtazama kwa jicho la dharau.

Enyi wananchi wapendwa! Mimi sikutoa maelezo haya mbele yenu ili niwaumizeni au kuvunja moyo wenu, bali kwa nia njema kabisa nataka kueleza kuwa mataifa yale yaliyoshika tabia hii na kujichagulia njia hii katika dini yao isiyojuzu ya kuwataja Manabii wa dini zingine kwa lugha mbaya na kuwatusi, siyo tu ni

7 Aali'Imraan, 3:85

wenye dhambi mbele ya Mungu kwa mwingiliano wao usiotakikana ambao hawana uthibitisho, bali wanayo pia ile dhambi ya kupanda mbegu ya unafiki na uadui katika wanadamu. Jipe moyo, unipe jibu la jambo hili kuwa kama mtu fulani amtukane baba ya mtu mwingine au amsingizie tuhuma mama yake, je haishambulii heshima ya baba yake mwenyewe? Na yule mtu anayetukanwa hivyo akijibu kwa tusi vilevile, je haitakuwa sawa kusema kwamba kwa kweli chanzo cha matusi hayo ya kulipiza ni yule mtu aliyetangulia kutukana, na katika hali hii yeye mwenyewe atakuwa adui wa heshima ya baba na mama yake.

Mwenyezi Mungu, ndani ya Kurani Tukufu, Ametufundisha somo la adabu na khulka kiasi hiki kwamba Anasema:

وَلَا تَسُبُّوا الَّذِينَ يَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ فَيَسُبُّوا اللَّهَ عَدْوًا بِغَيْرِ عِلْمٍ [8]

Yaani, nyinyi hata masanamu ya washirikina pia msiyatukane, kwani wao watamtukana Mungu wenu, maana, wao hawamjui Mungu Huyu. Sasa hebu angalieni kwamba ingawaje kwa mujibu wa mafundisho ya Mungu masanamu si kitu chochote, hata hivyo Mungu Anawafundisha Waislamu khulka hii kuwa fungeni midomo yenu msiyaseme vibaya

[8] Al-An'aam, 6:109

masanamu pia, na waelekezeni kwa upole tu, isije wakihamaki wakamtukana Mungu, na nyinyi ndiyo mtakuwa sababu ya matusi hayo. Hivyo, hali zao zikoje watu hawa wanaomtukana Nabii huyu mwenye adhama wa Uislamu, na wanamtaja kwa maneno ya kumfedhehesha, na kwa njia za kinyama kabisa wanashambulia heshima yake na mienendo yake. Nabii huyo mtukufu ambaye kwa kutaja jina lake, wafalme wakubwa wa Islam wenye adhama hushuka kutoka viti vyao vya enzi na huinama kwa kuzitii amri zake, na hujiona kuwa miongoni mwa watumwa wake wadogo, je heshima hiyo siyo kutoka kwa Mungu? Kuhakirisha heshima iliyotolewa na Mungu ni kitendo cha watu wanaotaka kupigana na Mungu. Hadhrat Muhammad Mustafaa[saw] ni yule mtukufu, mteule, Mjumbe wa Mungu, ambaye kwa kudhihirisha heshima yake na kusaidiwa kwake, Mungu Ameonyesha mifano mikubwa mikubwa. Je hii siyo kazi ya mkono wa Mungu uliowainamisha watu milioni mia mbili kwenye kizingiti chake. Ingawa kila Nabii anazo dalili kadhaa za kuthibitisha ukweli wake, lakini dalili nyingi za uthibitisho wa Unabii wake zinazoendelea kudhihirika hadi leo mfano wake haupatikani kwa Nabii mwingine yeyote awaye.

Eti ninyi hamwezi kuifahamu hoja hii! kuwa ardhi

inapochafuka na kunajisika kwa dhambi na katika mizani ya Mungu, maovu, mienendo mibaya na ukavu wa macho vinapoyazidi matendo mema, ndipo rehema ya Mungu inadai kuwa katika wakati kama huo, ufisadi wa ardhii uondolewe kwa kumtuma mja Wake. Maradhi yanahitaji tabibu. Na nyinyi mnaweza sana kuliko wengine wote kulielewa jambo hili, kwani kulingana na kauli zenu Veda haikuja wakati wa kuwapo tufani ya madhambi, bali ilikuja wakati ule ambapo ardhini hakukuwa na mafuriko ya madhambi. Basi, je kwa mtazamo wenu jambo hili haliyumkiniki kuwa Nabii adhihiri ambapo mafuriko ya madhambi yanaendelea kwa kasi kubwa katika kila nchi.

Mimi sidhani kuwa ninyi mtakuwa hamna habari ya tukio hili la kihistoria kuwa Mtume wetu[saw] alipojaaliwa kuwa Mtume, zama zile zilikuwa zama za giza kiasi hiki kwamba katika sehemu yoyote ya duniani iliyokaliwa na watu hakuna sehemu isiyokuwa na mwenendo mbaya na itikadi mbovu. Na kama vile Pandit Dayanad anaandika ndani ya kitabu chake *Sat'yarth Parkaash* kwamba katika zama hizo ndani ya nchi hii ya India pia ibada ya masanamu ilichukua mahali pa ibada ya Mungu, na uharibifu mwingi katika dini ya Veda ulikuwa umetokea.

Vivyo hivyo Padri Pfander — matamshi Fander —

mwandishi wa kitabu cha M*izanul Haq,* ambaye ni mtetezi mkubwa wa dini ya Kikristo na ni Mwingereza wa Ulaya, yeye anaandika katika kitabu chake *Mizanul Haq* kuwa katika zama za ujaji wa Mtume Mtukufu[saw] taifa la Kikristo lilikuwa limeharibika zaidi kuliko mataifa yote na mienendo yake mibaya ilikuwa ni fedheha na aibu kwa dini ya Kikristo. Na Kurani Tukufu yenyewe pia katika kuelezea haja ya kushuka kwake imeleta Aya hii:

ظَهَرَ الْفَسَادُ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ [9]

yaani misitu ikaharibika na mito pia ikaharibika. Muradi wa aya hii ni kuwa hakuna taifa lolote lile hata kama lilikuwa na hali za kikatili au hata kama lilikuwa na madai ya kuwa na akili sana halikuepukana na ufisadi.

Sasa, ithibitikapo kwa shuhuda zote kuwa watu wa zama za Mtume Mtukufu[saw], wa Mashariki kwa wa Magharibi, wakazi wa nchi ya India kwa wakazi wa jangwa la Uarabu, na hata wale waishio katika visiwa, wote hao walikuwa wameharibika, na hakukuwepo hata mmoja aliyekuwa na mahusiano mazuri na Mungu. Na matendo mabaya yalichafua ardhi. Basi, je mtu mwenye akili hawezi kufahamu kuwa huo ulikuwa ndio wakati na hizo zilikuwa ni zama ambazo

[9] Ar-Ruum, 30:42

akili ingeweza kupendekeza kuwa katika zama za giza kama hizo ilikuwa inatakiwa lazima angekuja Nabii mwenye shani kubwa.

Swali linabakia hili kuwa Nabii huyu baada ya kuja duniani amefanya marekebisho gani? Jibu la swali hili kuhusiana na marekebisho aliyofanya Mtume[saw] jinsi Mwislamu anavyoweza kutoa, nasema kwa nguvu sana kuwa jibu zuri na lenye hoja nzito kiasi hiki hakuna awezaye kutoa Mkristo yeyote, wala Myahudi, wala Mwaria yeyote.

Shabaha ya kwanza ya Mtume Mtukufu[saw] ilikuwa ni kuirekebisha Bara Arabu. Kuhusiana na hali ya nchi za Waarabu wakati ule ilikuwa vigumu kusema kwamba walikuwa wanadamu. Ni uovu gani walioukosa, na ni ushirikina gani usiokuwa ndani mwao. Wizi na ujambazi ulikuwa ni kazi yao. Kwao kumwaga damu bila haki kulikuwa ni kitendo cha kawaida sana kama vile kumkanyaga sisimizi chini ya mguu. Wakiwaua watoto mayatima, wakala mali zao; waliwazika watoto wa kike wakiwa hai; zinaa waliionea fahari na wakaeleza mambo hayo machafu hadharani katika mashairi yao. Ulevi ndani ya taifa hilo ulikithiri kiasi kwamba hakuna nyumba yoyote iliyokuwa haina pombe, na katika kamari walizidi kuliko nchi zote. Walikuwa wabaya zaidi kuliko wanyama na wabovu kuliko nyoka na mbwa mwitu.

Kisha Mtume wetu[saw] alipoinuka kwa ajili ya kuwarekebisha, na kwa mwelekeo wake wa batini akadhamiria kuitakasa mioyo yao, basi katika muda mfupi tu kukatokea ndani ya mioyo yao mabadiliko, wakawa wanadamu kutoka hali yao ya unyama, kisha kutoka wanadamu wa kawaida wakawa watu waliostaarabika, na kutoka watu waliostaarabika wakawa waja wa Mungu. Na hatimaye wakajipoteza ndani ya mapenzi ya Mwenyezi Mungu hata kwamba wakavumilia kila mateso mfano wa kiungo kisichokuwa na hisia. Waliadhibiwa kwa namna mbalimbali, walipigwa mijeledi bila huruma, walilazwa juani juu ya mchanga moto moto, walifungwa, walinyimwa chakula na maji mpaka wakafa, lakini wakati wa kila msiba wakasonga mbele. Na walikuwepo wengi miongoni mwao ambao watoto wao waliuawa mbele ya macho yao, na walikuwepo wengi waliouawa msalabani mbele ya watoto wao. Na jinsi walivyotoa uhai wao katika njia ya Mungu kwa ukweli wa moyo, kuifikiri tu kunaliza. Kama si utawala wa Mungu na athari ya mwelekeo wa Nabii wake ndani ya mioyo yao, basi ni kitu gani kilichowavutia kwenye Uislamu, na kwa kuletea mabadiliko yasiyo ya kawaida kikawahamasisha waangukie kizingiti chake yule ambaye alikuwa masikini hohehahe, asiye na mali, alikuwa akizunguka

peke yake katika mitaa ya Makka. Kwa vyovyote kulikuwa na nguvu fulani ya kiroho iliyowapeleka juu kutoka chini. Na jambo la kushangaza zaidi ni hili kuwa wengi wao katika hali ya ukafiri walikuwa maadui wakali sana wa Mtume[saw] na walikuwa na hamu ya kumwaga damu yake. Basi mimi sioni mwujiza mkubwa zaidi kuliko huu kuwa mtu mmoja muflisi hohehahe alivyoitakasa mioyo yao na kila aina ya chuki na kuwavutia kwake mpaka wakayatupa mavazi yao ya fahari, wakivaa nguo hafifu za kawaida kabisa wakahudhuria kumtumikia.

Baadhi ya watu wasiofahamu wanailaumu Islam kuhusiana na jihad na wanasema kuwa watu hao wote walisilimishwa kwa nguvu ya upanga. Ni Masikitiko mara elfu kuwa hao wamevuka mipaka katika udhalimu na kuficha haki. Hae, nasikitika, wamepatwa na nini kwamba kwa makusudi wanapuuza matukio sahihi. Mtume wetu[saw] hakudhihiri Uarabuni kama mfalme hata idhaniwe kwamba kwa vile alikuwa na nguvu na shani ya kifalme, hivyo watu walikusanyika chini ya bendera yake kwa ajili ya kusalimisha uhai wao.

Basi, swali lenyewe ni hili kuwa alipotoa mwito kuhusiana na Umoja wa Mungu na Utume wake katika hali yake ya ufukara na umaskini na upweke, wakati huo kwa hofu ya upanga gani watu

walimwamini; na kama watu hawakumwamini, basi kwa ajili ya kuwalazimisha, mfalme gani aliombwa kuleta jeshi na kusaidia? Enyi watafutao ukweli!! Eleweni kwa yakini kuwa maneno haya yote ni uzushi wa watu wale ambao ni maadui wakali wa dini ya Kiislamu. Isomeni historia kuwa Mtume Mtukufu[saw] ni yule mtoto yatima ambaye baba yake alifariki siku chache baada ya yeye kuzaliwa, na mama yake alifariki alipokuwa mtoto wa miezi michache. Hapo huyo mtoto ambaye Mkono wa Mungu ulikuwa pamoja naye aliendelea kulelewa katika ulinzi wa Mungu bila kumtegemea mtu. Na katika siku hizo za shida na uyatima aliwahi pia kuchunga mbuzi wa baadhi ya watu, na hakuwa na mlezi yeyote isipokuwa Mungu tu na hata baada ya kufikia umri wa miaka ishirini na mitano hata baba mdogo yeyote hakumwozesha binti yake, kwani kama ilivyoonekana kwa dhahiri, yeye asingeweza kuhimili matumizi ya nyumbani, na vile vile alikuwa hajui kusoma wala kuandika, wala hakujua ufundi wowote wala kazi yoyote. Kisha alipofikia umri wa miaka arobaini, mara moja moyo wake ukavutika kwa Mungu. Pango moja liko maili chache kutoka Makka liitwalo Hiraa, yeye akawa anaenda huko peke yake na kukaa faraghani ndani ya pango hilo na kumkumbuka Mungu. Siku moja ndani ya pango hilo alipokuwa anafanya ibada hali ya kuwa

faraghani, ndipo Mwenyezi Mungu Akamdhihirikia, naye akaagizwa kwamba kwa kuwa dunia imeiacha njia ya Mungu, na ardhi imechafuka na dhambi, hivyo Mimi ninakutuma wewe kuwa Mjumbe Wangu, sasa wewe watanabahishe watu kuwa wamwelekee Mungu kabla ya kufika adhabu. Yeye akisikia amri hii akaogopa kuwa miye *Ummi* yaani mtu nisiyejua kusoma wala kuandika, na akasema kuwa mimi sijui kusoma. Ndipo Mungu Akamjaza kifuani mwake elimu zote za kiroho na akaung'arisha moyo wake. Kwa athari za nguvu yake takatifu watu maskini na wanyonge wakaanza kumjia wakiwa watifu wake. Na wale watu waliokuwa wakubwa wakubwa wakajikaza kumfanyia uadui mpaka hapo mwishoni walitaka kumwua. Na wanaume na wanawake kadhaa wakauawa kwa kuteswa sana. Na shambulio la mwisho walilolifanya ni kwamba wakaizingira nyumba yake kwa ajili ya kumwua Mtume Mtukufu[saw]. Lakini nani aweza kumwua yule ambaye Mugnu anamlinda? Mungu kwa wahyi wake Akamwambia kuwa uondoke katika mji huu na Mimi nitakuwa pamoja nawe katika hatua zote. Ndipo akaondoka Makka pamoja na Abu Bakr r.a., wakajificha ndani ya pango la Thaur kwa siku tatu. Maadui wakamfuata wakimchukua mpelezi mmoja mpaka wakafikia kwenye pango. Yule mpelelezi

akafikisha alama za miguu mpaka kwenye pango, na akawaambia mtafuteni ndani ya pango hili, mbele hakuna alama tena za miguu. Na kama alienda mbele, basi huenda akapaa mbinguni. Lakini nani anaweza kuyawekea kikomo maajabu ya kudra za Mungu. Katika usiku mmoja tu Mungu Akaonyesha kudra yake kuwa buibui kwa utando wake akaziba mlango wote wa pango, na njiwa mmoja akajenga kiota na kutaga mayai. Na yule mpelelezi alipowashawishi watu waingie ndani ya pango, mzee mmoja akasema kuwa mpelelezi huyu amepatwa na kichaa. Mimi ninauona utando huu mlangoni pa pango tangu kabla hajazaliwa Muhammad^saw^. Kwa kusikia maneno hayo watu wote wakatawanyika na wakaachilia mbali wazo la pango.

Baadaye Mtume Mtukufu^saw^ akawasili Madina kisirisiri, na watu wengi wa Madina wakamkubali. Hapo hasira za watu wa Makka zikalipuka, na wakasikitika kuwa windo letu limetuponyoka. Sasa nini kilichofuata!! Ni kwamba wakashughulikia kupanga mipango jinsi ya kumwua Mtume Mtukufu^saw^. Na watu wachache waliomwamini Mtume^saw^ hao nao kutoka Makka walihamia nchi mbalimbali. Baadhi yao wakaomba hifadhi kwa Mfalme wa Uhabeshi. Baadhi yao wakabaki humo humo Makka kwa kukosa masurufu ya safari, hao

wakateswa sana. Maelezo yao yamo ndani ya Kurani Tukufu jinsi walivyoendelea kuomba msaada kwa vilio usiku na mchana.

Na dhuluma za Makuraishi zilipita kiasi na wakaanza kuwaua wanawake na watoto mayatima, na baadhi ya wanawake waliwaua kwa ukatili usio na huruma kiasi hiki kwamba miguu yao miwili ilifungwa kamba mbili, na kamba hizo zilifungwa kwa nguvu kwa ngamia wawili, kisha ngamia hao wawili wakakimbizwa kwenye pande mbili tofauti, basi wanawake hao wakachanika vipande viwili, wakafa.

Dhuluma za makafiri wakatili zilipofikia hatua hii, ndipo Mungu Ambaye hatimaye Anawahurumia waja wake Akamfunulia wahyi Mtume wake kuwa vilio vya waliodhulumiwa vimenifikia. Leo natoa idhini kuwa nyinyi pia pambaneni nao, na kumbukeni kuwa wale wanaoinua upanga dhidi ya watu wasio na hatia, hao watauawa kwa upanga tu, lakini nyinyi msipate kupita kiasi, maana Mungu  Hawafanyi marafiki wale wanaopita kiasi.

Huu ndio uhakika wa jihadi ya Kiislamu ambayo kwa dhuluma kubwa imeelezwa kwa njia mbaya. Hamna shaka kuwa Mungu ni Mpole, lakini shari ya taifa lolote inapopita kiasi, hapo Yeye huwa hamwachi mdhalimu bila kumwadhibu, na Huandaa Mwenyewe

sababu za maangamizi ya taifa hilo.

Mimi sijui wapinzani wetu wamesikia kutoka wapi na kwa nani kuwa Islam ilienea kwa nguvu ya upanga? Mungu Anasema ndani ya Kurani Tukufu:

لَآ اِكۡرَاهَ فِي الدِّيۡنِ[10]

Yaani, hakuna kulazimisha ndani ya Islam. Sasa ni nani aliyetoa agizo la kulazimisha, na njia za kulazimisha zilikuwa ni zipi? Na je wale wanaolazimishwa kusilimu, ikhlasi na imani yao ndiyo inakuwa kwamba bila kupata malipo yoyote, watu mia mbili, tatu wanapambana na maelfu ya watu, na wanapofikia elfu moja waweze kuwashinda maadui malaki kadhaa, na kwa ajili ya kuilinda dini kutokana na mashambulizi ya maadui wajitolee kukatwa vichwa vyao kama kondoo na mbuzi, na wagonge mihuri ya ukweli wa Uislamu kwa damu zao, na kwa ajili ya kueneza umoja wa Mungu wawe na mapenzi ya kujitolea kiasi hiki kwamba kidaruweshi wakivumilia taabu wafike hadi majangwa ya Afrika na kueneza Uislamu nchini humo. Na kisha wakipata kila aina ya usumbufu wafike mpaka China, siyo kwa kupigana vita, bali kwa njia ya kujitolea tu kidaruweshi, na wakifika katika nchi hiyo wawaite watu kwenye dini ya Kiislamu, na matokeo yake yawe

[10] Al-Baqara, 2:257

kwamba kwa mawaidha yao yenye baraka, mamilioni ya Waislamu wapatikane katika ardhi hiyo. Kisha waje katika India wenye kujivalia nguo za kawaida za kidaruweshi, na sehemu kubwa ya Bara Hindi waipatie heshima ya kusilimu, na sauti ya لَآ اِلٰهَ اِلَّا اللهُ wafikishe mpaka Ulaya! Semeni kwa imani, je hiyo ni kazi ya wale watu ambao wanasilimishwa kwa nguvu ambao mioyo yao ni kafiri, na ulimi wao ni mumini? Hapana. Bali hizi ni kazi za wale ambao mioyo yao hujaa nuru ya imani, na ambao ndani ya mioyo yao huwa Mungu tu pekee.

Tena tunarejea upande huu kuwa mafundisho ya Uislamu ni nini? Iwe wazi kuwa shabaha kubwa ya Uislamu ni kuimarisha Umoja wa Mungu na jalali yake duniani na kuing'oa kabisa ushirikina, na kwa kuleta madhehebu yote kwenye *Kalima* moja kuwafanya kuwa taifa moja. Dini zote zilizokuja duniani na manabii na mitumo wote waliokuja duniani, mtazamo wao uliishia kwa taifa lao na kwa nchi yao tu. Na kama walifundisha khulka kadhaa, shabaha ya mafundisho ya khulka haikuwa zaidi ya kwamba walinufaishe taifa lao tu kwa khulka zao. Ndiyo maana Hadhrat Masihi[as] alisema waziwazi kuwa mafundisho yangu yanawahusu wana wa Israeli tu, na pale mwanamke mmoja ambaye hakuwa wa

nyumba wa Israeli alipomwomba mwongozo, kwa unyenyekevu mkubwa akamkatalia. Kisha yule mwanamke maskini akajifananisha na mbwa jike na akaomba tena mwongozo, lakini akapewa jibu lile lile kuwa mimi nimetumwa kwa kondoo wa Israeli. Basi yule mama akanyamaza. Lakini Mtume wetu[saw] hakusema popote kuwa mimi nimekuja kwa ajili ya Waarabu tu, bali imo ndani ya Kurani Tukufu:

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا[11]

Yaani, waambie watu kuwa mimi nimetumwa kwa ajili ya dunia nzima. Lakini ikumbukwe kuwa Hadhrat Isa[as] kumkatalia mwanamke yule kwa uwazi halikuwa jambo la dhambi ya Nabii Isa[as], bali zama za mwongozo wa watu wote zilikuwa hazijafika, na Mungu Alimpa Nabii Isa[as] maagizo haya kuwa wewe umetumwa mahususi kwa ajili ya Waisraeli, wengine huhusiki nao kabisa.

Hivyo, kama nilivyosema sasa hivi mafundisho ya kikhulka ya Nabii Isa[as] pia yalikuwa yanaishia kwa Wayahudi tu. Sababu yake ni kuwa ndani ya Torati mlikuwa na maamrisho haya kuwa malipo ya jino ni jino, malipo ya jicho ni jicho na malipo ya pua ni pua; na shabaha ya mafundisho haya ilikuwa ni kuimarisha uadilifu ndani ya Wayahudi na kuwazuia uonevu.

---

[11] Al-A'raaf, 7:159

Kwa vile hao waliishi katika hali ya utumwa zaidi ya miaka mia nne, sifa za dhuluma na uonevu zilikuwa zimezaliana ndani yao, hivyo hekima ya Mungu ikataka kuwa kama vile kulipa kisasi kulikuwa na nguvu sana katika tabia zao, basi kuondoa hali ile ililazimu mafundisho ya kikhulka yatolewe kwa nguvu ile ile. Na mafundisho hayo ya kikhulka ndiyo Injili ambayo ni kwa Wayahudi tu siyo kwa ajili ya dunia nzima, maana Hadhrat Isa[as] hakuhusika hata kidogo na mataifa mengine.

Lakini kweli yenyewe ni kuwa ndani ya mafundisho yale aliyoyaleta Hadhrat Isa[as] hamkuwa na kasoro hii tu kuwa hayakuwa na msingi wa huruma kwa watu wote, bali kasoro nyingine ni hii pia kwamba kama vile kuhusu mafundisho ya ukali na kulipa kisasi Torati ilivyoelekea kuzidisha nguvu kupita kiasi, vivyo hivyo Injili kuhusu mafundisho ya kusamehe ilivyoinamia sana kupita kiasi kwenye msamaha. Vitabu hivyo viwili havikuyajali matawi yote ya mti wa kibinadamu. Bali, Torati inataja tawi moja tu la mti huo na tawi la pili lipo mkononi  mwa Injili, na mafundisho yote mawili hayapo ya wasitani. Kwani kama vile kila wakati na kila mahali kulipa kisasi na kutoa adhabu siyo busara, vivyo hivyo kila wakati na kila mara kumsamehe na kumwachia mtu kosa lake ni kinyume kabisa cha taratibu ya malezi. Ni kwa sababu

hiyo, Kurani Tukufu imeyakataa mafundisho haya mawili na kusema:

جَزَٰٓؤُا۟ سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِّثْلُهَا ۚ فَمَنْ عَفَا وَأَصْلَحَ فَأَجْرُهُۥ عَلَى ٱللَّهِ [12]

Yaani, malipo ya ubaya ni kadri ya ubaya uliofanywa - sawa na mafundisho ya Torati yalivyo - lakini mtu ambaye asamehe  kama vile ni mafundisho ya Injili, basi katika hali hii msamaha utapendeza na utajuzu ikiwa matokeo yake mema yanatokea; na aliyesamehewa, kujirekebisha kwake kunatarajiwa kwa msamaha huo. Lakini kanuni ni ile ile iliyotajwa ndani ya Torati.

[12] Ash-Shuuraa, 42:41